

SURA YA TISA TAMAA YA MAKUU

“Akili bila tamaa ya makuu ni ndege bila mabawa” Salvador Dali. Mark Twain alisema, “ Kaa mbali na wale ambao wanadharau tamaa yako ya makuu. Watu wadogo hufanya hivyo lakini watu mashuhuri hukufanya wewe uamini kuwa na wewe pia unaweza kuwa mashuhuri.”

Hakuna kitu chochote kikubwa au mashuhuri kilichotokea kuwepo bila kuwepo mtu mwenye tamaa ya makuu nyuma yake. **Yaani mwenye tamaa ya kufanya mambo yasiyokuwa ya kawaida. Hii ni tamaa yakutoka katika kufanya vitu vidogo, au vya wastani na kufanya vitu vikubwa** Tamaa ya makuu ina maana ya hitaji la nguvu la kufanya au kupata vitu vikubwa au tuseme visivyo vya kawaida katika maisha. Inakufanya wewe ulenge kitu maalumu na cha maana katika maisha yako. Kwa kweli unaamua kubadilisha historia ya maisha yako kwa kufanya vitu vikubwa badala ya vitu ambavyo vinafanywa na wengi. Tamaa itakupa mwelekeo na hamasa ya kuelekea kwenye lengo kuu katika maisha. Ili kupanda na kuwa mtu maarufu duniani ni lazima uwe na tamaa ya kufanya mambo yasiyo ya kawaida kwako hivyo wewe unakuwa ni chachu ya kubadilisha hali ilivyo. Tamaa hiyo ndiyo mama wa mambo yote mazuri na yakuvutia duniani, na ndiyo chanzo cha uboreshaji wa mambo.

Kwa hivyo tamaaambayo iko nje ya maadili ya kutaka kupata vitu kwa njia ya mkato ni hatari kwani yaweza kuhatarisha maisha yako, kukuumiza na hata kukufanya ukaanza kusumbuka mno na hata kupoteza maisha.

Hata hivyo ni ukweli kuwa tamaa ya makuu ina matokeo chanya mengi kuliko hasi. Kitu cha kujua ni kuwa hakuna awezaye kufanikiwa mambo makubwa bila kuchipuka tamaa ya makuu. Jay Leno alisema, **“Tamaa ya makuu hupiga akili kwa asilimia 99 wakati wote.”** Ni vizuri kupenda kuwa zaidi au kujua zaidi au kufanya zaidi na kutoa zaidi.

Na hivyo kuwa na malengo na msukumo mkubwa utakaokufanya ufika mbali na kuvipata vyote unavyovilenga vikiwa ni vya aina ya pekee. Unalazimika kuanza huota zaidi na kufikiria makubwa kwa sababu ya tamaa kuu ambayo unayona itakuongoza kutimiza ndoto zako kuu. John Stuart Millalisema, **“ni vizuri zaidi kuwa binadamu usiyeridhika, kuliko kuwa nguruwe uliyeridhika ni vizuri zaidi kuwa Socrates usiyeridhika kuliko kuwa mjinga uliyeridhika.”**

Tamaa ya makuu ni nyenzo muhimu kwa mafanikio yako , ndiyo inayoongoza vipaji na hata rasilimali. Unakapokuwa na tamaakubwa unapata uwezo wa kuelekea kwenye mambo makubwa naya kuridhisha. Wewe hutaweza kuangalia magumu ya mbele. Ni kwa vile ile tamaa imejaa ndani ya moyo na akili itakupa msukumo. Na hivyo ndoto na ujasiri wa kufanya mambo makubwa duniani itakufikisha mbali. **Ndiyo maana unaweza kuwa na kipaji, elimu kubwa na hata ujuzi lakini kama huna tamaa ya makuu utaishia kuwa mtu wa kawaida na mwenye mafanikio ya kawaida tu.** Wapo watu wengi katika jamii na wewe hushangaa kwa vile hukutegemea wawe kama walivyo. Ni kwa vile hawakuwa na tamaa ya kufanya mambo makubwa na hivyo wapakoteza uwezo na nguvu zao. William Faulkner alisema, **“kila wakati ota na lenga juu zaidi kuliko unavyojua unaweza. Usihangaike kuwa bora kuliko wenzako au waliokutangulia. Jaribu kuwa bora kuliko wewe mwenyewe”.**